RISALA YA UTII YA WANANCHI WA WILAYA YA KIGAMBONI KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MH. SAMIA SULUHU HASSAN KWENYE MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2021
WILAYA YA KIGAMBONI TAREHE 21 - 22/ 08/ 2021

2.0 UTANGULIZI

Mhe. Rais, Viongozi na Wananchi wa Wilaya ya Kigamboni tunayo furaha na heshima kubwa kuwakaribisha Vijana shupavu wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2021, katika Wilaya yetu ya Kigamboni **'KARIBUNI SANA WILAYA YA KIGAMBONI'.**

2.1 UJUMBE WA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2021

Mhe. Rais, Tumepokea Ujumbe wa Mbio Maalum za Mwenge wa Uhuru mwaka 2021 unaohusu Maendeleo ya Sekta ya Tehama chini ya kauli mbiu:- **"TEHAMA ni msingi wa Taifa endelevu; itumie kwa usahihi na Uwajibikaji.**

Mhe. Rais, TEHAMA ni teknolojia ya habari na mawasiliano inayotumika kwa ajili ya kusambaza, kuhifadhi, kuunda, kushirikiana, kupashana habari na kurahisisha miamala ya fedha. Faida za matumizi ya TEHAMA ni pamoja na kurahisisha mawasiliano, kuboresha makusanyo ya Serikali na kudhibiti uvujaji wa mapato ya Serikali.

Mhe. Rais, Matumizi ya TEHAMA yamekua na msaada mkubwa katika kuboresha takwimu za Kitaifa na kutoa vitambulisho vya Taifa, wananchi wa Wilaya ya Kigamboni wanaendelea kujiandikisha kupata vitambulisho vya Taifa kwa matumizi mbalimbali ikiwemo usajili wa namba za simu, na kwa utambuzi wa uraia wa muhusika.

Mhe. Rais, Makadirio ya kuandikisha wananchi wenye umri wa miaka 18 na zaidi kwa mwaka 2020/2021 ndani ya Wilaya ya Kigamboni ilikua watu 56000, hadi kufikia Juni, 2021 wananchi waliokwisha sajiliwa katika mfumo wa NIDA ni 34162 na wote wana namba za utambulisho na wameshapatiwa vitambulisho vyao. Makadirio ya kuandikisha watoto chini ya miaka 5 kwa ajili ya kupatiwa vyeti vya kuzaliwa kwa mwaka 2020/2021 ilikua ni 20760 hadi kufikia mwezi Juni, 2021 watoto walioandikishwa na kupatiwa vyeti ni 10975 sawa na 52.8%.

Mhe. Rais, Wananchi wa Kigamboni wengi wao ni wakulima (12082), wavuvi (2147) na wafanyabiashara (4284) na wanatumia simu zao kwa kupiga, kutuma ujumbe mfupi "SMS", kuingia kwenye mitandao ya kijamii kama 'Whatsapp', 'Facebook', 'Twiter' na 'Instagram' kwa kutafuta masoko, bei za Kimataifa na Kitaifa na kwa biashara nyingine mbalimbali na kufanya miamala ya kifedha.

Mhe. Rais, Wananchi wa Wilaya ya Kigamboni wanao uelewa wa kutosha kuhusu faida za matumizi ya TEHAMA kutokana na kuwepo kwa ongezeko la wakala wa huduma za kifedha kwa njia ya mtandao ambapo kwa sasa kuna jumla ya mawakala 102 wa Tigo-pesa, Airtel Money, Z-pesa, T-pesa, M-pesa na mawakala wa benki za NMB na CRDB.

Mhe. Rais, Wananchi wanatumia fursa za TEHAMA katika masuala ya ajira, Vijana wengi wamejiajiri katika Sanaa ya Matangazo (Graphics Design) kupitia TEHAMA kwani biashara zote zinahitaji kujitangaza. Utengenezaji wa Tovuti mbalimbali kwa kuwa tovuti ni ofisi pekee inayoweza kufikiwa na mteja akiwa popote pale duniani.

Mhe. Rais, Wilaya ya Kigamboni inatekeleza matumizi ya TEHAMA kwa ustawi wa wananchi na Taifa kwa kupitia sekta mbalimbali kama ifuatavyo:-

2.1 Sekta ya Elimu.

Mhe. Rais, Mfumo wa taarifa za kifedha FFARS umeunganishwa katika shule zote za Serikali (Msingi 34 na Sekondari 15) ili kusimamia na kudhibiti matumizi ya kila siku ya fedha za umma. Mfumo wa taarifa za elimu PREMS/PREM ambao hutumika kupata taarifa na takwimu za wanafunzi. Mfumo huu pia umerahisisha na kupunguza muda uliokuwa ukitumika katika masuala ya uhamisho wa wanafunzi kutoka shule moja kwenda nyingine.

2.2 Sekta ya Afya:

Mhe. Rais, Wilaya inatumia mifumo ya FFARS, GoTHOMIS, MTUHA, ViMIS, TiMR na PlanRep. FFARS unatumika kwenye vituo vyote 22 kwa kusimamia, kudhibiti matumizi ya kila siku na kutoa taarifa mbalimbali za matumizi ya fedha ngazi ya kituo. GoTHOMIS unatumika kwenye vituo 5 kwa makusanyo ya maduhuli na kudhibiti matumizi. MTUHA unatumika kwenye vituo vyote 22 kwa kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati na kuongeza tija katika ufanyaji wa kazi kwa kujipima na umewezesha kukagua ubora wa taarifa za Afya kwenye vituo vya kutolea huduma. ViMS unatumika kwenye vituo vyote 22 kwa kuagiza chanjo ngazi ya Mkoa na kuzisambaza pamoja na kutoa taarifa za watoto waliochanjwa. TiMR unatumika kwenye vituo vyote 22 kwa kuagiza chanjo na PlanRep unatumika kwenye vituo vyote 22 kwa kuandaa mipango ya bajeti na taarifa mbalimbali. Mifumo hii imeongeza ufanisi katika usimamizi wa huduma za afya.

2.3 Sekta ya Ujenzi:

Mhe. Rais, Wakala wa barabara za Vijijini na Mijini – TARURA hutumia mifumo mitatu ya TEHAMA, kwanza DROMAS (District Roads Management System) ambao husaidia Taasisi katika kutunza taarifa mbalimbali za mtandao wa barabara, kupanga matengenezo ya barabara kwa kila mwaka na kutoa taarifa mbalimbali za kibajeti, mfumo wa pili ni MUSE (Mfumo wa ulipaji serikalini) mfumo ambao hutumika kufanya malipo yote ndani ya Taasisi na mfumo wa tatu ni TeRMIS (TARURA e-Revenue Management Information System) ambao hutumika kukusanyia tozo za maegesho kwenye hifadhi za barabara

2.4 Sekta ya Maji:

Mhe. Rais, Wakala wa Maji Mijini na Usafi wa Mazingira (DAWASA) hutumia mfumo wa "RSDMS" ambao hutumika kwa ajili ya kuandaa taarifa za miradi na kuzituma Wizarani kwa urahisi na kwa wakati, pia baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Kigamboni wanapokea ankara za maji na kufanya malipo kwa njia ya simu, hivyo imeweza kuongeza ufanisi wa ukusanyaji mapato na kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha.

2.5 Sekta ya Maendeleo ya Jamii:

Mhe. Rais, Mfumo wa *"CMG REGISTRATION SYSTEM"* umerahisisha utumaji wa maombi ya usajili ambapo kwa sasa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha vinaweza kufanya maombi kwa njia ya mtandao bila kufika katika ofisi ya usajili ngazi ya Halmashauri, hadi kufikia Juni, 2021 jumla ya vikundi 62 vimesajiliwa kupitia mfumo wa 'CMG'. Kupitia mradi wa TASAF III, Walengwa kaya 234 kati ya walengwa 964 wa kaya maskini wanapokea ruzuku kwa njia ya simu za mkononi katika mitandao ya TIGO PESA, M-PESA, AIRTEL MONEY na Z- PESA. Utaratibu huu umesaidia kufikisha ruzuku kwa usalama na kwa wakati.

2.6 Malipo ya Tozo Mbalimbali Serikalini:

Mhe. Rais, Katika idara za Mazingira, Maliasili, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ardhi, Ujenzi, Fedha na Biashara na Taasisi za Maji (DAWASA) na Umeme (TANESCO), Mfumo wa malipo

wa kielektroniki umewezesha wananchi kufanya malipo popote walipo baada ya kuwa na namba ya udhibiti wa malipo "*control number*". Hii imerahisisha katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kuzuia mianya ya upotevu wa mapato na kuweza kuongeza ukusanyaji wa mapato.

2.7 Ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri:

Mhe. Rais, Kupitia Mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato (LGRCIS) na mashine za kukusanyia mapato za PoS, Wilaya imeongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kutoka shs 3,432,340,089.00 mwaka 2016/2017 kabla ya mfumo hadi shs 8,487,415,365.56 kwa mwaka 2020/2021 baada ya mfumo kusimikwa. Mfumo umesaidia kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali.

2.8 Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao:

Mhe. Rais, Jeshi la Polisi hutuma na kupokea taarifa mbalimbali kwa njia ya mtandao ikiwemo simu za masafa marefu na redio za mawimbi mafupi (digital redio call), kupitia kwenye makundi ya "whatsapp" na pia kupitia GPS zinazofungwa kwenye vyombo vya usafiri na vyombo vya ndani vya umeme kama luninga (TV) na redio, hivyo taarifa za kiutendaji na maelekezo yanapatikana kwa urahisi na haraka kwa kupitia TEHAMA na kuweza kufuatilia mali zilizoibiwa.

3.0 UKAMILISHAJI NA UENDELEVU WA MIRADI ILIYOPITIWA NA MBIO ZA MWENGE MWAKA 2019

Mhe. Rais, Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2019 ulipitia jumla ya miradi mitano (**5)** katika kata nne (**4)** (Vijibweni, Kibada, Mjimwema na Somangila) kwa kukagua na kuzindua miradi ya maendeleo mitano (**5)** katika sekta ya Afya miwili (**2)**, Elimu Msingi mmoja (**1)**, Viwanda (Kiwanda cha Vifungashio) mmoja (**1)** na Sekta ya Maji mmoja (**1)**. Miradi mitatu (**3)** ilizinduliwa na miradi miwili (**2)** ilikaguliwa. Miradi yote mitano (**5)** iligharimu shilingi **13,814,718,625.33** mpaka kukamilika ambapo Serikali Kuu ilichangia shilingi **194,071,460.00**, Halmashauri shilingi **262,647,165.33** na Wafadhili shilingi **13,358,000,000.00.** Miradi mitatu (**3**) iliyozinduliwa ni pamoja na madarasa mawili (**2**) katika shule ya Msingi Vijibweni ambayo yanatumika, uzinduzi wa kiwanda cha Vifungashio ambacho hadi sasa kinaendelea kutoa huduma na uzinduzi wa jengo la mionzi (X-Rays) katika Hospitali ya Vijibweni, jengo linatumika na huduma zinatolewa. Miradi iliyokaguliwa ni ya ujenzi wa chuo cha afya Kigamboni na ukarabati wa mradi wa maji Gezaulole, miradi yote hii inaendelea kutoa huduma hadi sasa.

4.0 MIRADI YA MAENDELEO KATIKA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2021

Mhe. Rais, Mwenge wa Uhuru 2021 Wilayani Kigamboni umekimbizwa kilometa 82.3 katika Tarafa tatu (3) (Kigamboni, Somangila na Pembamnazi) na Kata tano (5) (Vijibweni, Kigamboni, Mjimwema, Somangila na Kimbiji) na umepitia miradi ya maendeleo ya ujenzi mitano (5) katika Sekta za Afya miradi miwili (Uwekaji mawe ya msingi katika miradi ya ujenzi wa Zahanati na Jengo la Mionzi katika Kituo cha afya Kimbiji), Elimu miradi miwili (Uzinduzi wa Jengo la Ofisi ya Uthibiti Ubora wa Elimu na Uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa Bweni la Wanawake shule ya Sekondari Kimbiji) na Barabara mradi mmoja (Ujenzi wa Barabara ya Azimio – Mashujaa yenye urefu wa kilomita 1,46) na kukagua shughuli za mradi wa kikundi cha VEMA na mradi mmoja (1) uliopitiwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru za mwaka 2019 (Ukarabati wa Kisima cha Maji Gezaulole)

Mhe. Rais, Miradi iliyopitiwa na Mwenge wa Uhuru mwaka 2021 ina thamani ya Sh. 1,306,469,431.75 zikiwemo Sh. 31,110,000.00 za michango na nguvu za wananchi, Sh. 113,226,829.64 za Mapato ya Ndani ya Halmashauri na Sh. 1,162,132,602.11 fedha toka Serikali Kuu.

Aidha kwenye uwanja wa mkesha Mwenge wa Uhuru mwaka 2021 umekagua mabanda mbalimbali ya shughuli za Kiuchumi na Kijamii ikiwemo mabanda ya mapambano dhidi ya dawa za Kulevya, mapambano dhidi ya Malaria, TAKUKURU, Vikundi vya Kiuchumi, Mfuko wa Afya ya Jamii, masuala ya Lishe, mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI, TEHAMA, Watu wenye Ulemavu na Maonyesho ya shughuli za Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

4.1 Kiasi cha Fedha kilichochangwa kwa ajili ya shughuli za Mbio Maalum za Mwenge Uhuru Mwaka 2021

Mhe. Rais, Hadi kufikia tarehe 15/08/2021, jumla ya sh. 49,775,000.00 taslimu zimechangwa kwa ajili ya shughuli za Mbio Maalum za Mwenge wa Uhuru mwaka 2021 ambapo Wadau wamechangia sh. 45,000,000.00 na Manispaa ya Kigamboni sh. 4,775,000.00

5.0 UTEKELEZAJI WA UJUMBE WA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2021

5.1 MAPAMBANO DHIDI YA VVU/UKIMWI

Mhe. Rais, Tumeupokea ujumbe wa VVU/UKIMWI chini ya kauli mbiu isemayo:- ***"Mshikamano wa Kitaifa, Tuwajibike kwa pamoja"***. Hali ya maambukizi katika Wilaya ya Kigamboni imepungua kutoka 6.0% mwaka 2016 hadi 4.0% mwaka 2020. Elimu ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI inatolewa katika Vituo vyote 41 vya huduma za afya kila siku. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya wananchi waliojitokeza kupima VVU na kupewa ushauri nasaha walikuwa ni 3,778 (me – 1565 na ke - 2213) kati yao waliokutwa na maambukizi mapya ya VVU ni 120 sawa na asilimia 3.1 ya wote waliopimwa.

Mhe. Rais, Katika vituo vyote vya kutolea huduma za Afya ikiwemo Hospitali ya Wilaya, vituo vya Afya na Zahanati kuna vitendanishi vya upimaji vya kutosha. Pia vituo vina dawa za kufubaza VVU, wenye mahitaji maalum wanafikishiwa dawa katika maeneo yao na wataalam wa huduma za VVU majumbani ambapo jumla ya watu 35,485 (me 11,377 na ke 24,108) wanapata huduma.

Mhe. Rais, Kwa mwaka 2020 /2021 kina mama wajawazito 3888 walipimwa virusi vya UKIMWI, kati ya hao waliokutwa na maambukizi ni 66, sawa na asilimia 1.6 ya waliopimwa na wakapatiwa ushauri nasaha ili kuzuia maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto. Aidha, kati ya watoto 2,401 waliozaliwa, watoto 3 chini ya miaka mitano sawa na asilimia 0.1 walikuwa na maambukizi ya VVU.

Mhe. Rais, Wilaya inashirikiana na wadau mbalimbali yakiwemo mashirika ya **MDH, FHI 360, MUKIKUTE, WASO, TAYOHUG, KIPENET na KIYODEN** katika kutekeleza afua mbalimbali za kupambana na maambukizi ya VVU/UKIMWI, pia Vikundi vya sanaa na wasanii binafsi wanashiriki kutoa elimu kupitia mabonanza yanayofanyika katika ngazi za Mitaa, Kata na Wilaya.

5.2 MAPAMBANO DHIDI YA MALARIA

Mhe. Rais, Tumeupokea ujumbe wa Malaria chini ya kauli mbiu isemayo:- ***"Ziro Malaria inaanza na Mimi- Nachukua hatua kuitokomeza"*** **.** Ugonjwa wa Malaria kwa sasa umepungua kwa kiasi kikubwa, na kwa sasa ni ugonjwa wa tisa (9) kati ya magonjwa kumi yanayosumbua wananchi wa Wilaya ya Kigamboni toka ilipokua namba 1 kwa mwaka 2016. Wagonjwa wa Malaria wamepungua toka wagonjwa 12,029 mwaka 2019 sawa na 5.5% ya watu 216,611 waliopima mpaka wagonjwa 10,822 mwaka 2020 sawa na 3.4% ya watu 318,012 waliopima. Pia vifo vilivyosababishwa na ugonjwa wa malaria vimepungua kwa 100% kwa mwaka 2020 kutoka vifo saba 7 mwaka 2017.

Mhe Rais, Katika kupambana na Malaria, Wilaya ililenga kunyunyizia dawa za kuua mazalia ya mbu waenezao Malaria katika madimbwi 70. Jumla ya lita 1000 za dawa aina ya BACTIVEC zilinyunyiziwa katika madimbwi 50 katika Kata tano (5) (Tungi, Kigamboni, Vijibweni, Somangila na Mjimwema) kwa mwaka 2020 kwa gharama ya sh. 39,600,000.00, fedha toka Serikali Kuu.

Mhe Rais, Wilaya imeendelea kushirikiana na wadau wa Double 'S' Furmigation, Safi Furmigation na Mkombozi Furmigation katika kupambana na maambukizi ya malaria kwa kuua mbu pevu katika makazi ya watu kwa ajili ya kupunguza maambukizi.

5.3 MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA

Mhe Rais, Tumeupokea ujumbe wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya chini ya kauli mbiu isemayo:- **"Elimu sahihi juu ya Dawa za Kulevya huboresha huduma kwa Waraibu; chukua hatua".** Wilaya ya Kigamboni imekuwa ikitoa huduma kwa Waathirika wa dawa za kulevya kwa baadhi ya vituo vya afya na Hospitali zetu. Pia, Wilaya ina nyumba 10 za upataji nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya ambazo zinamilikiwa na Watu binafsi, chini ya mwongozo wa Mamlaka ya Dawa za Kulevya Tanzania. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 jumla wa waathirika 1945 walipatiwa matibabu

Mhe. Rais, Uongozi wa Wilaya kwa kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama unaendelea na mapambano dhidi ya matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya ambapo kuanzia Januari hadi Julai, 2020 watuhumiwa 36 wa madawa ya kulevya aina ya bangi walikamatwa na kilogram 4.67 za bangi. Jumla ya kesi 20 zilifikishwa Mahakamani na baadhi ya watuhumiwa walihukumiwa. Aidha kwa mwaka husika, mtuhumiwa mmoja (1) alikamatwa na mirungi na mwingine mmoja (1) alikamatwa na Heroin. Kesi mbili (2) (moja ya mirungi na nyingine ya Heroin) zimefikishwa mahakamani. Kwa mwaka 2021, kuanzia Januari hadi Julai, 2021 jumla ya watuhumiwa 43 walikamatwa na kilogram 5.48 za bangi na jumla ya kesi 22 zipo Mahakamani na nyingine zipo hatua ya upelelezi. Aidha, kwa kipindi hicho husika, watuhumiwa wawili (2) walikamatwa na kilogram 4.76 za mirungi na kesi moja kufikishwa Mahakamani.

Mhe. Rais, Elimu inayohusiana na madhara ya dawa za kulevya imekuwa ikitolewa katika maeneo ya Mashuleni, minadani, kwenye vituo vya daladala na bodaboda, kwenye maeneo ya Wavuvi na ndani ya vituo vyote vya Afya. Pia, Wilaya imejenga Kituo cha kutoa huduma za madawa ya kulevya katika Hospitali ya Vijibweni kwa kuhudumia watu wa jinsi zote na kuzingatia miundombinu kwa watu wenye ulemavu. Huduma ya urekebishaji tabia zilizojitokeza kwa kutumia dawa za kulevya na kujifunza mbinu za kuboresha uchumi kwa mtu mmoja mmoja hutolewa kituoni hapo. Pia katika Wilaya kuna Asasi za **TAYOHAG, TEWWY** na **MKIKUTE** ambazo zinaendelea kutoa elimu inayohusiana na dawa za kulevya.

5.4 MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA

Mhe Rais, Tumeupokea ujumbe wa Rushwa chini ya kauli mbiu isemayo:- **"Kupambana na Rushwa ni Jukumu langu** ". Kwa kutambua umuhimu wa kuzuia na kupambana na vitendo vya Rushwa kwa mwaka 2020/2021 Wilaya ya Kigamboni yalipokelewa malalamiko 121 kutoka Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma, watumishi na watu binafsi na hadi kufikia mwezi Juni, 2021 uchunguzi wa malalamiko nane (8) unaendelea kufanyika. Majalada 55 yamefunguliwa, kesi tano (5) zimefunguliwa, kesi mbili (2) Serikali imeshinda na kesi tatu (3) zinaendelea Mahakamani.

Mhe. Rais, Ili kuhakikisha panakuwepo na miradi endelevu ndani ya Wilaya, TAKUKURU imefanya ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa ili kuona inaendana na thamani halisi ya fedha zilizotolewa. Jumla ya miradi nane (8) ilikaguliwa katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Mhe. Rais, Wilaya inatambua umuhimu wa Jamii kuendelea kupatiwa elimu juu ya madhara ya rushwa, mwaka 2020 jumla ya Semina 23 zilifanyika, Vilabu 30 vya wapinga Rushwa vilifunguliwa na vilabu 56 kuimarishwa na Mikutano ya hadhara 25 ilifanyika katika maeneo mbalimbali wilayani. Pia maonyesho 3 yamefanyika na makala 5 zilitolewa.

5.5 LISHE BORA KWA AFYA IMARA

Mhe. Rais, Tumeupokea ujumbe wa lishe bora kwa afya imara wenye kauli mbiu isemayo:- **"Tujenge jamii yenye Afya Imara kwa kuzingatia lishe bora".** Wilaya ya Kigamboni ina asilimia 0.4% ya watoto chini ya miaka mitano wenye utapiamlo mkali na asilimia 2.5 ya wanawake wajawazito wana upungufu wa damu.

Mhe. Rais, Kupitia watoa huduma wa afya 67 ngazi ya jamii wenye mafunzo ya lishe na watoa huduma wa afya vituoni wamewasaidia wananchi kuelewa dalili za utapiamlo, jinsi ya kujiepusha na utapiamlo na namna bora za kupata huduma ya afya.

Mhe. Rais, Wazazi na walezi wamehamasika katika kuhakikisha watoto wanapata lishe kwa kipindi cha siku elfu moja kwani utapiamlo mkali umeshuka kutoka asilimia 0.6 kwa mawaka 2019/2020 mpaka 0.4 kwa mwaka 2020/2021. Na watoto waliopatiwa matone ya Vitamin A wameongezeka kutoa asilimia 99% kwa mwaka 2019/2020 mpaka asilimia 100 kwa mwaka 2020/2021. Pia asilimia 83.34 ya wajawazito walitumia vidonge vya kuongeza damu kwa mwaka 2020/2021.

6.0. HITIMISHO

Mhe. Rais, pamoja na shukrani zetu kubwa kwako sisi Wananchi wa Wilaya ya Kigamboni tunatekeleza kwa vitendo ujumbe wa Mwenge wa Uhuru wenye kaulimbiu **"TEHAMA ni msingi wa Taifa endelevu; itumie kwa usahihi na Uwajibikaji"**.

Mwisho kwa niaba ya Uongozi wa Wilaya tunawatakia Vijana wote wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka, 2021 heri na baraka katika kufanikisha jukumu hili kubwa walilokabidhiwa na Taifa letu.

Mhe. Rais, Risala hii pia imeambatishwa na viambata 'A – R' vinavyohusu Taarifa za miradi na shughuli zilizopitiwa na Mbio Maalum za Mwenge wa Uhuru mwaka 2021.

Naomba kuwasilisha.

MWENGE WA UHURU OYEEE!!!!

Fatma A. Nyangasa
MKUU WA WILAYA KIGAMBONI